


# Zab. 79 - Tazama mzabibu wako


Mziki wa Jeannot Amani Mulume

♩ = 65



Ta - za-ma m-za-bi-bu wa-ko Bwa - na, u-je ku-o-ko-a ta - i-fa la - ko.

5 B $\flat$  E $\flat$  B $\flat$  Gm C7 F B $\flat$  Dm Gm7 C7m F



## Shairi: 9-10, 13-14, 15-16, 19-20

1. Ulingoa mzabibu toka Misri,  
ukawafukuza mataifa, ukaupanda;  
kwake ukapalia udongo, tayari,  
nao ukatoa mizizi, ukaijaza n-chi.
2. Kwa nini umebomoa kuta zake,  
ili wote wanaopita njiani wachume zabibu zake?  
Ili nguruwe wa mwituni auharibu,  
na wanyama wa porini wautafune?
3. Ee Mungu wa majeshi, urudi,  
uongalie toka mbinguni, uone,  
uje kutazama mzabibu huo.  
Uulinde huo uliopanda kwa mkono wako wa kuume.
4. Hatutakuacha tena hata kidogo;  
utatutunzia maisha, nasi tutamba jina lako.  
Ee Bwana, Mungu wa majeshi, utusimike tena,  
uangazishe uso wako, nasi tutaokoka.